

**MTIHANI WA MWIGO
KARATASI YA KWANZA
MUDA: SAA 2**

MWONGOZO WA INSHA

1.

- a) Mtahiniwa afafanue maana ya mitandao ya kijamii.
Atoe njia ambazo mitandao ya kijamii imeleta mabadiliko makubwa maishani.
Ajadili kwa kina mabadiliko yanayoletwa na mitandao ya kijamii.
Atoe mapendekezo yake kuhusu mabadiliko yanayoletwa na mitandao ya kijamii.
(Tanbihi: sio lazima mwafunzi afafanue maana ya mitandao ya kijamii).
- b) Sura ya ratiba
 - Anwani
 - Mahali pa sherehe
 - Tarehe
 - Saa/ wakati wa kila shughuli
 - Wahusika /wasimamizi wa kila shughuli mbalimbali zinafanywa na wakati wa kufanyika
 - Vishemu – saa / wakati / shughuli na wahusika / wasimamizi.
- c) Mtahiniwa aeleze maana ya juu na ndani (si lazima).
 - Mtahiniwa atoe kisa / visa kuthibitisha au atoe kisa cha moja kwa moja. Mf: Mtu ambaye hali yake ilikuwa duni wakati mmoja akaimarika / akatajirika na watu wakaanza kuchunguza kiini cha utajiri wake bila kuamini angeweza kufanikiwa hivyo kwa bidii yake.
- d) Insha irejelee mambo yalijiriri baada ya juu kutua.
 - Aonyeshe shughuli za mchana na vile alishinda siku nzima.
 - Kisa kiwe cha kuvutia
 - Atumie lugha sanifu na msamiati ufaao.

2. UFAHAMU

- a) **Kichwa mwafaka kwa taarifa hii**
Baa la njaa (alama 1)
- b) **Kwa mujibu wa taarifa hii, eleza sababu zinazosababisha baa la njaa nchini Kenya.**
- Ukame
- Ukutima duni
- Kuzoea misaada
- Mafuriko
- Ardhi duni (sababu za kihistoria) (zozote 4 x 1 = alama 4)
- c) **Pendekeza njia zozote tano za kuzuia njaa nchini.**
- Matumizi ya teknolojia ya kisasa
- Kula vyakula aina tofauti tofauti
- Kuimarishe miundo msingi
- Sera za ugawaji mashamba ziboreshwwe
- Mbinu bora za usambasaji wa nguvu za umeme, maji na usafiri bora.
- Kukuza vyakula nya kiasili k.v ndizi, mihogo n.k. (zozote 5 x 1 = alama 5)
- d) **Kwa maoni yako, eleza jinsi wanafunzi kutika vyuo vya walimu wanavyoweza kuchangia njaa nchini Kenya**
- Kuhamasisha umma
- Kwa kufanya utafiti
- Kushiriki katika upanzi wa miti na kutunza mazingira
- Kuzuia mmonyoko wa udongo
- Kufunza wananchi kuhusu kuepuka matumizi mabaya ya rasilimali.
- Kukuza uzalendo
- e) **Eleza athari za baa la njaa kwa nchi.**
- Gharama kubwa ya matibabu (utapia mlo.)
- Kukosa hadhi au heshima kimataifa
- Kuzorota kwa uchumi
- Kuporomoka kwa miundo msingi (zozote 3 x 1 = alama 3)
- f) Eleza maana ya maneno haya kwa mujibu wa taarifa
(i) Anuwai – aina aina
(ii) Viunga – sehemu iliyoota mitit au matunda (2 x 1 = alama 2)

3. MATUMIZI YA LUGHA

- a. **Andika maana mbili za sentensi hii:**

Mtu mwenye kofia ni jirani yangu.

- Mtu mwenye cheo

- Mtu aliyeaa vazi litwalo kofia

(2 x 1 = alama 2)

b. Tambulisha viambishi na mzizi katika neno:

Wanakaa

- Wa – nafsi
- Na – wakati
- Ka – mzizi
- A – kiishio

(4 x 1/2 = alama 2)

c. Andika kwa wingi.

Ua huu mrefu unaizingira nyumba.

Nyua hizi ndefu zinazingira nyumba

(alama 2)

d. Andika kwa kufuata maagizo:

Nani amezipoteza funguo zako? Anza: Funguo..

Funguo zako zimepotezwa na nani?

(1 x 2 = alama 2)

e. Tumia – baya – kama kivumishi katika sentensi.

Tathmini sentensi za wanafunzi

k.m Mtoto mbyaya hulia mara kwa mara.

Kiti kibaya kimetupwa

N + V

(1 x 2 = alama 2)

f. Onyesha kundi Nomino na kundi Tenzi katika sentensi ifuatayo:

Alivumilia mpaka mwisho

- KN –
- KT – Alivumilia mpaka mwisho
(Sentensi hii haina KN).

(2 x 1 = alama 2)

g. Andika sentensi moja ili kuonyeasha matumizi ya hali isiyodhihirika.

Hali isiyodhihirika ni “a”

K.m Ala chakula.

Mwizi afungua jela miak kumi

(1 x 2 = alama 2)

h. Kanusha sentensi ifuatayo.

Mchezo utakapokuwa ukiendelea, mashabiki watakuwa wakishangilia

Mchezo utakapokuwa haundelei, mshabiki hawatakuwa wakishangilia.

(alama 2)

i. Bainisha kitenzi katika sentensi ifuatayo na ueleze ni cha aina gani.

Yule ndiye mwenye matunda haya.

Ndiye – kitenzi kishirikishi kipungufu

(1 x 2 = alama 2)

j. Tunga sentensi yenyenye muundo ufuatao

W+ T +H + N

Tathmini sentensi za wanafunzi

Yule alikaa nyuma ya nyumba.

W T H N

(4 x 1/2 = alama 2)

k. Sentensi ifuatayo ni ya aina gani?

Kijana njoo

Sentensi sahihi

(alama 1)

l. Andika kiunganishi kinachoonyesha majuto

K.M Laiti, Lau, Kama, falaula, ila

(alama 1)

m. Kwa kutoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi.

Irabu pekee k.m oa, ua

Konsonanti pekee k.m mtu

Konsonanti mwambatano ng'ombe, kunywa

Konsonanti + irabu k.m baba

(alama 2)

n. Andika kifungu kifuatacho katika usemi halisi.

Karema alimsihi mama yake amruhusu kwanza adurusu masomo yake halafu ajifulie

nguo. Mama yake alimpa saa moja

“Mama niruhusu kwanza nidurusu masoma yangu halafu / kasha nijifulie nguo.” Karema akaomba. “Nimekupa saa moja,” Mama akajibu.

(8 x 1/2 = alama 4)

o. Taja nomino za jamii za maneno yafuatayo:

Ndizi

Mkungu wa ndizi / fungu / chane

Kuni

Tita la kuni

(2 x 1 = alama 2)

4. MATUMIZI YA LUGHA

A. Andkia jibu la salamu hii: alamsiki (alama 2)

Binuru / Alamsiki

B. Tegua kitendawili hiki: Mbona mwaandamana hata na kina babu na mizigo, safari ya wapi?

Siafu

(alama 2)

C. Methali ifuatayo inatoa ushauri gani? (alama 2)

Kumcha Mungu si kilemba cheupe

Usiangalie umbile / wajihii/ mavazi kama kielezo cha tabia au hali ya mtu.

D. Godoro ni kwa kitanda na zulia ni kwa (alama 1)

Sakafu

E. Anapofungiwa mshukiwa huitwa (alama 1)

Ramande/ seli

F. Watu hawa hufanya kazi gani? (alama 2)

i) **Mnyapara**

Msimamizi wa utekelezaji wa kazi fulani

ii) **Sarahangi**

Mtu wa pili baada ya nahodha, naibu anayesimamia mabaharia katika chombo

G. Kapu la kubeba matunda huitwa (alama 2)

Pakacha

- | | |
|---|------------------|
| H. Sikio ni kwa kusikiliza, figo ni kwa | (alama 1) |
| Kuchuja, kusafisha damu | |
| I. Mwewe, Kipanga ni aina ya ndege ambaye hunyakua vifaranga | (alama 1) |
| Ghuba / Hori/ Komeo | |
| J. Sehemu kubwa ya bahari iliyoingia ndani ya pwani huitwa | (alama 1) |
| Kishanfu / hazama / kikero | |
| K. Pambo ambalo huvaliwa kwenye uti wa pua huitwa | (alama 1) |
| Kishanfu / hazama / kikero | |
| L. Andika kisawe cha: | |
| i) Kabumbu | |
| Soka, kandanda | |
| ii) Mwanasesere | |
| Mwanaabudu, abudu, doli | |
| | (alama 2) |
| M. Bunda ni kwa karatasi, kicha ni kwa funguo ilhali Bumba/ wingu ni kwa nzige | |
| | (alama 2) |

5. SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA (ALAMA 10)

Huku ukitoa mifano, eleza sifa za kimsingi zinazotambulisha sajili ya mazungumzo ya kawaida

- Kukatizana usemi
- Lugha ya majibizano
- Sentensi fupi fupi hutumika
- Kuhamisha misimbo
- Utohozi
- Kusitasita
- Kukamilishiana uneni

- Uradidi / kurudiarudia maneno
- Matumizi ya ishara
- Mada hubadilikabadilika
- Kutomalisha sentensi
- Dayolojia – mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi
- Matumizi ya ucheshi na utani
- Matumizi ya usemi halisi
- Kutumia chuku au kutia usemi chumvi
- Alama za dukuduku hutumika kuonyesha kauli isiyokamilika.
- Kuchanganya ndimi.

(zozote 10 x 1 = alama 10)